

UAINISHAJI WA KIMOFOLAJIA WA NGELI ZA NOMINO ZA KISWAHILI

R. Mgullu

Utangulizi

Lengo mahsusi la makala haya ni kuonyesha jinsi nomino za Kiswahili zinavyoweza kuainishwa katika ngeli kwa kuzingatia maumbo ya viambishi awali vya nomino, yaani Kimafolojia. Utaratibu wa uainishaji huo utachambuliwa. Udhaifu unaojitokeza katika kazi za awali utajadiliwa. Hatimaye tutapendekeza utaratibu mwingine ambao unaweza kutumiwa wakati wa kuziainisha Nomino za Kiswahili katika ngeli za kimofolojia.

Dhana ya Ngeli za Nomino

Dhana ya ngeli si mpya katika uwanja wa Isimu, isipokuwa labda istilahi yenyewe ya *ngeli* ndiyo ambayo inaonekana kuwa ni mpya katika lugha ya Kiswahili. Kapinga (1983) anaeleza ya kuwa istilahi ya ngeli umechukuliwa kutoka lugha ya Kihaya. Katika lugha ya Kihaya neno ngeli lina maana ya aina ya kitu. Kwa mantiki hiyo, ngeli inakuwa na maana ya "*kundi la nomino za aina moja.*"

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981) nayo inaeleza kuwa:

"Ngeli' (ji) ni:

Utaratibu wa taaluma ya sarufi ya lugha katika kupanga aina za majina (nomino) k.v., ki, vi, ma, n.kl

Hatuyaungi mkono maelezo haya. Tunaamini ya kuwa ngeli ni kundi la nomino za aina moja na si ule utaratibu wa kuzipanga nomino katika makundi (ngeli). Tuki (1990) wanaeleza ya kuwa:

Ngeli nomino ni:

Kundi moja la majina yaliyo na upatanisho wa kisarufi unaofanana na viambishi vya umoja na wingi vinavyofanana".

Nusu tunayaunga mkono maelezo haya na nusu tunatofautiana nayo. Kwa mujibu wa maelezo haya ngeli itakuwa na nomino zilizizo na upatanisho wa kisarufi unaofanana (na hiki ni kigezo cha kisintaksia na siyo cha kimofolojia) na pia nomino hizo ziwe na viambishi awali vinavyofanana (Hiki ni kigezo (mwega) cha kimofolojia).

Kwa maoni yetu, vigezo hivi viwili haviwezi kutumika kwa pamoja na ndiyo maana makala yetu inasema “Uainishaji wa kimofolojia”. Hatuingizi masuala ya kisintaksia (k.v, upatanisho) katika uainishaji huu. Wachambuzi wa awali waliojaribu kutumia vigezo vyote kwa pamoja walishindwa. Hii ni sababu mojawapo ambayo imefanya uainishaji wa ngeli za nomino za Kiswahili uwe wa kutatanisha. Kwa hiyo tunaamini ya kuwa lugha ya Kiswahili inayo mifumo miwili ya ngeli za nomino. Mfumo moja ni wa kimofolojia na mwingine ni wa kisintaksia.

Utaratibu wa kuziainisha nomino katika ngeli kwa kutumia viambishi awali vya nomino umekuwa ukitumiwa na wanaisimu wengi kuainishia ngeli za nomino za lugha hasa za kibantu ikiwa ni pamoja na Kiswahili. Kwa mujibu wa kigezo hiki nomino zote zilizozitokeza na viambishi awali vya umoja au uwingi vinavyofanana huwekwa katika kundi moja ambalo huitwa *NGELI* (Noun Class) (Meinhof 1948.). “Kwa hiyo, ngeli ya nomino ni kundi la nomino zenye viambishi awali vya umoja na/au uwingi vinavyofanana. Kwa mujibu wa kigezo hiki, suala la ngeli linakuwa ni suala la kimofolojia.

Ngeli hupangwa kwa kuzingatia maumbo (mofolojia) ya nomino. Kwa mantiki hiyo nomino kama. Kijana - vijana, kitabu - vitabu, kiwete - viwete; kiongozi - viongozi, ipo katika ngeli moja kimofolojia kwani zote zina kiambishi awali *ki* cha umoja na kiambishi *vi* cha uwingi. Baadhi ya wanaisimu walioshughulikia uainishaji wa kimofolojia wa ngeli za nomino za Kiswahili ni pamoja na Krapf (1850), Madan (1884/1921); Ashton (1944); Meinhof (1910); Guthrie (1948/1967); Brain (1969); Loogman (1965); Polome (1867); De Wolf (1971); Steere (1934/1976); na Myachina (1981). Kazi zao zitajadiliwa katika sehemu ya tatu ya makala haya.

Pamoja na ukweli ya kuwa wanaisimu wote waliotajwa hapo juu walikutumia kigezo kilekile cha mofolojia katika uainishaji wao wa ngeli za nomino za Kiswahili, lakini, zipo tofauti nyingi zilizojitokeza katika uainishaji wao. Tofauti hizo ndio ambazo huzua utata mkubwa ambao umelikumba suala zima la ngeli za nomino za Kiswahili. Suala la ngeli za nomino za Kiswahili sasa hivi linaonekana kuwa ni suala linaloteleza. Kutokana na utata huo, mwandishi wa makala haya aliona umuhimu wa kulitazama tena suala la ngeli za nomino za Kiswahili ili mchango wake usaidie katika kupunguza utata uliopo na ikiwezekana kuimaliza kabisa.

Nomino tulizotumia katika uainishaji huu ni zile zinazotumiwa katika mawasiliano ya kawaida (msamiati) na wala si istilahi. Aidha, nomino zilizotumiwa ni zile ambazo zimeorodheshwa kama vidahizo katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (1981). Mwandishi wa makala haya vilevile ametilia maanani maoni na mawazo yaliyotolewa na wazawa kadhaa wa lugha ya Kiswahili. Katika makala haya, hatutashughulikia uainishaji wa kisintaksia wa ngeli za nomino za Kiswahili.

Uchambuzi wa Awali wa Uainishaji wa Kimofolojia wa Ngeli za Nomino za Kiswahili

Ili tuweze kuzisawiri tofauti zilizojitokeza miongoni mwa wanaisimu walioziainisha kimofolojia ngeli za nomino za Kiswahili, tutatumia mifano ya miainisho iliyofanywa na wanaisimu Krapf (1850); Madan (1921); Ashton (1944); Brain (1969); Loogman (1965); Palome (1867); Steere (1934); na Myachina (1981). Tunaamini ya kuwa wanaisimu tuliowataja hapo juu wanawawakilisha wanaisimu wengine wa mkondo huu (ambao kazi zao hatutazijadili). Kazi zote hizi zilifanywa katika karne za kumi na tisa na ishirini.

Wanaisimu wanane waliotajwa hapo juu waliziainisha nomino za Kiswahili katika ngeli kama inavyoonyeshwa katika kielelezo cha kwanza hapa chini.

Mifano ya nomino katika kila ngeli

Kwa mujibu wa wanaisimu wa mkondo huu, nomino zilizostahili kuwekwa katika ngeli mbalimbali ni kama ifuatavyo:

1. NGELI YA M.= WA

1. M - toto -Wa - toto (M - Wa)
2. Mw - limu -Walimu (Mw - Wa)
3. Mu - ungwana -Wa - ungwanaa (Mu - Wa)

Kutokana na mifano yetu hapo juu, tunagundua ya kuwa kiambishi awali (M) cha umoja kinaweza kujidhihirisha katika maumbo mengine (tuyaite alomofu) yafuatayo: (i) (Mw) na (ii) (Mu).

2. NGELI YA M = MI

1. Mti - Miti (M - MI)
2. Mchungwa - Michungwa (M - Mi)
3. Mtume - Mitume (M - Mi)

3. NGELI YA JI/ Ø= MA

1. Jicho - Macho (Ji - Ma)
2. Kashaha - Makasha (Ø - Ma)
3. Balozi - Mabalozzi (Ø - Ma)

Tunapoichunguza mifano iliyotolewa katika ngeli hii, tunagundua ya kuwa kiambishi awali (Ji) cha umoja huweza pia kujidhihirisha kwa alomofu kama (Ø).

4. NGELI YA KI = VI

1. Kiti - Viti (Ki - Vi)
2. Chakula - Vyakula (Ch - Vy)
3. Kijana - Vijana (Ki - Vi)

Mfano (2) hapo juu unatuthibitishia ya kuwa kiambishi awali (KI) cha umoja huweza wakati mwingine kutokea kama alomofu (ch). Na kaiambisho awali vi cha wingi hutokea pia kama alomofu (vy).

5. NGELI YA U (MA)

1. Ufa - Nyufa (U - Ny)
2. Udevu - Ndevu (U - N)
3. Ugonjwa - magonjwa (U - Ma)
4. Uzuri - Uzuri (U - U)

Hapa, mifano inadhihirisha ya kuwa Nomino zinazowekwa katika ngeli hii zinatofautiana sana kimofolojia. Tutajadili zaidi katika sehemu ya tathmini ya uainishaji huu.

6. NGELI YA KU (VITENZI JINA)

Mifano

1. Kucheza
2. Kuimba Mifano hii inadhihirisha ya kuwa nomino ambazo uwekwa katika ngeli hii zinatokana na vitenzi.
3. Kuandika
4. Kulia

7. NGELI YA PA = MU = KU

1. Hapa / Hapo
2. Huku / Huko
3. Humu / Humo
4. Tanzania
5. Kenya.

Tathmini ya Uainishaji wa Kimofolojia wa Ngeli za Nomino za Kiswahili

Ama kwa hakika tathmini ya uainishaji wa kimofolojia wa ngeli za nomino za Kiswahili ni ngumu. Ugumu wa kuifanya tathmini hii unatokana na ukwele ya kwamba zipo tofauti nyingi za msingi zilizojitokeza kati ya wanaisimu walioifanya kazi hizo zionekane

kuwa ni za mashaka na zisizokuwa na uhakika. Hebu tuangalie baadhi ya tofauti hizo.

Idadi ya ngeli

Ni vigumu sana hadi leo kwa watu waliozisoma kazi za wanaisimu hawa kujua kwa uhakika idadi ya ngeli za nomino za Kiswahili. Kila mtaalamu anayo idadi yake. Sababu moja ya wanaisimu hawa kupata idadi tofauti ya ngeli imetokana na baadhi ya wanaisimu hawa, kwa mfano Krapf (1850), Madan (1884/1921), Brain (1969) na Loogman (1963) kuviweka viambishi vya umoja na wingi katika ngeli moja ambapo wanaisimu wengine, kwa mfano Ashton (1944), Polome (1867) na Myachina (1981), wameviweka viambishi awali vya umoja katika ngeli tofauti na viambishi awali vya wingi. Hivyo ngeli moja katika kila kundi la kwanza k.m. (M - WA) inakuwa sawa na ngeli mbili katika kundi la pili ambapo M ya umoja ni tofauti na (wa) (ya wingi) ingawa nomino ni hiyohiyo. Sababu ya pili ya kutofautiana kwa idadi ya ngeli ni kwamba baadhi ya wanaisimu wameziacha ngeli nyingine ama kwa makusudi au bila kujua. Kwa kuzingatia utaratibu uliotumiwa na mwanaisimu Meinhof (1941) na Guthrie (1948) kupanga ngeli za nomino za lugha za kibantu, Polome (1967) ameziacha ngeli za 12 na 13. Myachina (1981) naye ameziacha ngeli za 12, 13, na 14 kwa sababu ngeli hizo hazipo katika Kiswahili. Aidha wanaisimu Krapf (1980), Madan (1884) Brain (1969), Loogman (1965), na Steere (1934) hawana ngeli kwa nomino dhahania. Pia Loogman (1865) hana ngeli pekee kwa Ku ya vitenzijina. Kwa jumla sababu hizi pamoja na nyingine zimesababisha idadi ya ngeli zinazotolewa na wanasarufi mbalimbali kutofautiana mno. Kuwepo kwa tofauti hizi pia si jambo zuri kwani zinawatatanisha wale wanaojifunza.

Majina ya ngeli

Kwa jumla, wanaisimu tuliochunguza kazi zao wanazitaja ngeli kwa kutumia viambishi awali vya ngeli inayohusika. Aghalabu wanatumia kiambishi cha umoja na cha wingi k.m. ngeli KI - VI, JI - MA, n.k. Hata hivyo, tofauti kadhaa zimejitokeza. Kwa mfano, Steere (1936) amezitaja ngeli zake kwa kutumia viambishi vya wingi tu, (ngeli) ya *WA, MI, MA* n.k.) Cha ajabu ni kuwa ngeli ya nne ameiita ngeli ya *KI* na siyo ngeli ya *VI*. Sababu ya kufanya hivyo anajua mwenyewe. Pia wanaisimu wengine wametumia viambishi awali vitatu badala ya viwili kuitaja ngeli moja. Kwa mfano Krapf (1850), na Brain (1969) "wanaziita ngeli zao za sita kuwa ni ngeli za U - (N), MA. Hali hii inadokeza utenge mkubwa wa uainishaji wa ngeli, kwani ingawa nomino hizo zimewekwa katika ngeli moja lakini kwa kweli hizo ni nomino za ngeli mbili tofauti."

Mfuatano wa ngeli

Wanaismu walioshughulikia ngeli za nomino za Kiswahili wamependelea kuzitaja ngeli kwa kutumia namba mfuatano (ordinal), kwa mfano, ngeli ya kwanza (na ya pili) kwa ngeli ya M - WA, Ngeli ya tatu (na nne) kwa ngeli ya M - MI n.k. Njia hiyo imezua utata mwingi. Ni ngeli ipi iwe ya kwanza au ya pili au ya tatu, au ya kumi na sita? Hili nalo ni tatizo kwani wanaisimu hawa waliposhughulikia uainishaji wa ngeli za nomino za Kiswahili hawakuzipanga kwa mfumo mmoja. Tukiangalia kwa mfano, katika nafasi ya ngeli ya tatu (au 5/6) tunaona ya kwamba wanaisimu wanne yaani: Krapf (1850), Loogman (1965), Polome, (1967) na Myachina (1981) wameiweka ngeli ya JI - MA na Ashton (1944) ame iweka ngeli ya M - WA. Madan (1884 - 1921) na Brain (1969) wameiweka ngeli ya KI - VI. Hivyo, ngeli tatu au sita tofauti zimewekwa katika nafasi hiyo. Tukiangalia tena kwenye nafasi ya ngeli ya nne (7/8) tunaona ya kwamba wanaisimu watano Krapf (1850), Loogman (1865), Polome (1967), Steere (1934) na Myachina (1981) wameiweka ngeli ya KI - VI. Madan (1921) ame iweka ngeli ya N - N: Hivyo, ngeli nne tofauti zimewekwa katika nafasi moja. Tukiangalia tena katika nafasi ya ngeli ya tano (au 9/10) tunaona ya kwamba wanaisimu watano Krapf (1850), Ashton. (1944), Loogman (1865), Polome (1967) na Myachina, (1981) wameiweka ngeli ya N - N, Madan (1921), Brain (1969) na Steere (1934) wameiweka ngeli ya JI - MA kwenye nafasi hiyo hiyo. Kwa hakika hii ni vurugu. Kwa hali kama hii, ni vigumu sana mtu kuzungumzia (juu ya) ngeli ya tatu au ya nne au ya tano, n.k. kwani kila mtaalamu amezipanga ngeli kwa utaratibu wake. Kutokana na utata huo wanaisimu wameanza kujiuliza maswali kadhaa, kwa mfano: Je, ni lazima ngeli fulani iwe ya kwanza? Kama jibu ni ndiyo, Je, ni kwa sababu gani iwe ya kwanza? Je, ni kwa nini ngeli hiyo ni muhimu zaidi kuliko nyingine? Au, ni kwa nini ina nomino nyingi zaidi? Au ni kwa sababu gani nyingine za kiisimu (au kijamii) zinazoifanya ngeli hiyo ihalalishwe kuwa ya kwanza, ya pili, ya tatu hadi ya mwisho? Na kama hakuna sababu yoyote muhimu basi watu wanaweza kuzipanga ngeli kama wanavyopenda na hilo ndilo lililotokea.

Tofauti ya nomino katika ngeli moja

Tofauti nyingine ambayo imeonekana ni ile ya kila mwanaisimu kuwa na nomino tofauti anazoiweka katika ngeli ileile. Tukiangalia ngeli ambazo hukaliwa na nomino ambazo huanzia na U (tuita ngeli ya U) tunagundua ya kwamba:-

1. Krapf (1950) ameziweka nomino za kuhesabika tu zenye maumbo y- U - N kama ufa - Nyufa, Ua -Nyua n.k. pamoja na U - Ma kama Ugonjwa - Magonjwa, Uasi - Maasi n.k.
2. Madan (1921) ameziweka nomino zenye maumbo ya U - Ny tu kama ufa - nyufa, Unga Nyungo n.k.

3. Ashton (1944) ameigawa ngeli ya U katika ngeli mbili. Ngeli moja ameiita-U (LU_) ambazo ni nomino za vitu (yabisi) ambavyo ni tungamo au vyenye urefu viamishi vyake ni U - N - (Ø) kwa mfano, ukuta-kuta, ndevu - ndevu, ubao - mbao n.k.
4. Brain (1969) ameweka nomino zinazofanana na zile za Krapf (1850) zenye U - N au U - Ma (zote ni nomino zinazohesabika.
5. Loogman (1965) ameitenga ngeli ya U katika ngeli mbili tofauti. Ngeli moja akaiita U - N kwa nomino kama Ufa- Nyufa Ungo - Nyungo n.k. Nyingine akaiita U - MA kwa nomino kama Ugonjwa - Magonjwa, Uasi - Maasi n.k.
6. Polome (1967) ameigawa ngeli ya U katika ngeli mbili. Ya kwanza (ya 11) amesema ni ya vitu binafsi vilivyo zaidi ya viwili (na, hutofautiana na ngeli ya tano ambayo kitu kimoja kati ya viwili. Ngeli ya pili (ngeli ya 14) ameipa nomino zifuatazo:
 - (i) Nomino dhahania - ufalme, uzuri, n.k.
 - (ii) Nomino zenye umbo la U - MA - Ugonjwa - Magonjwa
 - (iii) Nomino zenye umbo la U - N/O - Kama devu - ndevu, ukuni - kuni. n.k.
7. Steere (1934) ameweka nomino zenye maumbo ya U - N tu kama Ufa - nyufa, devu - ndevu n.k.
8. Myachina (1981) hakuitenga ngeli ya U lakini ameiwekea nomino tofauti tofauti nyingi sana kwa mfano:-
 - (i) Nomino zenye maumbo ya U - N k.m. (Ufa- Nyua, n.k.
 - (ii) Nomino zenye maumbo ya U - MA (Ugonjwa - Magonjwa, Uasi - Maasi, n.k.
 - (iii) Nomino dhahania, kwa mfano, uzuri, ubaya, utoto, n.k.
 - (iv) Nomino zenye wingi/umoja tu k.m. -ugali,
 - (v) Nomino zinazotaja majina ya nchi, k.m. Ubelgiji, Uingereza, Ufaransa, n.k.

Ama kwa hakika, tofauti hizi ni kubwa kiasi kwamba mtu yeyote anayejaribu kusoma kazi za wanaisimu hawa iliaelewe, atashindwa, kwani kadiri atakavyosoma kazi nyingi zaidi ndivyo atakavyozidi kuchanganyikiwa.

Kukosa mahali pa kuziweka nomino nyingine

Tatizo jingine la utaratibu huu wa kugawa nomino katika ngeli kwa kutumia viambishi awali TU ni li le la kukosa mahali pa kuziweka nomino nyingi za Lugha ya Kiswahili.

Baada ya kuchunguza kwa makini maumbo ya nomino za Kiswahili tumegundua ya kwamba nomino nyingi za Kiswahili hazianzii na viambishi awali M, Wa, M, Mi, Ji, Ma, Ki, Vi, N, Ku, MU, KU, (pamoja na alomofu zavyo). Ushahidi unaonyesha ya kuwa nomino za Kiswahili zimetapakaa katika mfumo mzima wa alfabeti ya Kiswahili kuanzia A hadi Z. k.m. A = adui, athari, afya, ada. B = baba, balaa, bahati, C = chatu D = dawati, daraja, darasa. E = embe, eneo, eka. F =, fukara, fitina filimbi. - G = gereza, genge, gogo. GH =, -GHASIA, GHADHABU, GHALA. H = habari, hadithi, haiba I = ibada, ibara, ibilisi. J = jua, jabali, jalala. K = kaa - kabila, kaburi. L = laana, lulu, limau. M = mate. N = Nzi, Nzige, Nd = ndama - nduli. . O = onyo, ombi, orodha. P = Pweza, panya, pua. R = rutuba, rushwa, rangi; S = suala, swala, sungura. Sh = shule, shukurani - shuka. T = Twiga, tuzo, tunu. Th, = thumuni, thamani, thelathini. U = Unguja V = vita, vazi, vuli, W = waziri Y = yai, yaya, yatima, Z = zoezi, zizi, ziwa. Kwa hiyo, kama tutazingatia kwa makini kabisa viambishi awali vilivyotumiwa kuainishia ngeli za nomino za Kiswahili ni dhahiri kwamba tutakosa mahali pa kuziweka nomino nyingi za Kiswahili. Tunadhani hali hii imechangia kwa kiasi kikubwa kuwapo kwa ngeli kapu' (yaani ngeli iliyoitwa N - N) ambamo kwa kweli huwekwa nomino karibu zote ambazo hazianzi na viambishi awali vilivyotajwa hapo juu. Ngeli kapu ni ushahidi mwingine kwamba uainishaji huu kwa hakika una makengeza.

Tumezijiadili tofauti tano (4.1 - 4.5) hapo juu. Huu ni ushahidi wa kutosha kutudhihirishia udhaifu uliopo hivi sasa katika kazi ambazo zimeainisha ngeli za nomino za Kiswahili kimofolojia. Ni vizuri ngeli za nomino za Kiswahili ziainishwe kimofolojia. Lakini si vyema kuendelea kuwa na tofauti za uainishaji kama hizi zilizopo sasa. Katika sehemu inayofuata tunatoa vigezo na mapendekezo ya uainishaji wa kimofolojia wa ngeli za Kiswahili ambazo tunaamini yatasaidia kuondoa kabisa au kupunguza tofauti zilizopo hivi sasa.

Kigezo cha Kimofolojia

Nomino zinaweza na zimeweza kuainishwa katika ngeli kwa kutumia vigezo kadhaa, kwa mfano kigezo cha mofolojia ya nomino, kigezo cha upatanisho wa Kisarufi kati ya nomino na aina nyingine za maneno (Kigezo cha Kisintaksia) na hata kigezo cha maana za nomino (kigezo cha kisemantiki) Kigezo tunachokitumia kuziainishia ngeli za nomino katika makala haya ni cha kimofolojia. Tunatumia viambishi awali vya nomino. Tunachosisitiza hapa ni kuwa viambishi awali huwekwa mwanzoni mwa nomino ili kuashiria Umoja au. Wingi wa nomino hizo. Na viambishi awali hivyo ndivyo tunavyovitumia kuzigawa nomino katika ngeli. Mambo yafuatayo yanazingatiwa.

1. Patakuwepo mzizi wa nomino ambao utajitokeza katika umoja na wingi. (Sehemu isiyobadilika).

2. Kiambishi awali cha umoja kitakuwa tofauti na kiambishi awali cha wingi.
3. Wakati mwingine kiambishi (cha umoja au wingi) huwa na alomofu zake.
4. Wakati mwingine alomofu kapa huwakilisha kiambishi awali cha umoja au wingi.
5. Nomino nyingine hazina kiambisho awali chochote. Mofolojia ya nomino hizi haiashirii idadi ya umoja wala wingi.

Ngeli za Hamino za Kiswahili

Kwa kuzingatia viambishi awali vya nomino za Kiswahili tunaweza kuwa na makundi makuu manne ya ngeli za nomino za Kiswahili yaani:

- (1) Ngeli za nomino zilizo na viambishi awali vyote viwili yaani:
 - (i) Kiambishi awali cha Umoja na
 - (ii) Kiambishi awali cha Wingi.
- (2) Ngeli za nomino zilizo na kiambishi awali cha umoja tu pamoja na mofu kapa ya wingi.
- (3) Ngeli za nomino zilizo na kiambishi awali cha wingi tu pamoja na mofu kapa ya umoja.
- (4) Ngeli za nomino zisizo na kiambishi awali chochote.

Ngeli za nomino zenye viambishi awali viwili

Kundi la ngeli lililo kamili kuliko makundi mengine yote ni hili lenye nomino zilizo na viambishi awali viwili. Kiambishi awali kimoja huwakilisha umoja na kingine huwakilisha wingi. Katika kundi hili zipo ngeli za nomino zifuatazo:

1. Ngeli ya M - WA:

Mifano:

- | | | | |
|-----|-----------|---|---------------------|
| (1) | Mtoto | - | Watoto (M - WA) |
| (2) | Mwalimu | - | Walimu (MW - WA) |
| (3) | Muongwana | - | Waungwana (MU - WA) |

Tunaona hapa kuwa kiambishi cha umoja ni M ambacho katika nomino nyingine hudhihirika kama {M} au {MW}. Katika muktadha huu {MU} na {MW} ni alomofu za M.

2. Ngeli ya M - MI

Mifano

- | | | | |
|-----|----------|---|--------------------|
| (1) | Mti | - | Miti (M- MI) |
| (2) | Mchungwa | - | Machungwa (M - MI) |
| (3) | Mtume | - | Mitume (M - MI) |

Hapa kiambishi cha umoja ni {M} na cha wingi ni {MI}.

3. Ngeli ya JI - MA

Mifano

- | | | | |
|-----|-------|---|-------|
| (1) | Jicho | - | Macho |
| (2) | Jino | - | Meno |
| (3) | Jiwe | - | Mawe |

Hapa kiambishi cha umoja ni {JI} na kile cha wingi ni {MA}..

4. Ngeli ya KI - VI

Mifano

- | | | | |
|-----|---------|---|---------|
| (1) | Kiti | - | Viti |
| (2) | Kijana | - | Vijana |
| (3) | Chakula | - | Vyakula |

Katika ngeli hii Kiambishi awali Ki cha umoja hujidhihirisha pia kwa alomofu ch na kiambishi vi cha wingi hujidhihirisha pia kwa alomofu vy katika baadhi ya nomino (mfano 3 hapo juu unahusika).

5. Ngeli ya U = N

Mifano

- | | | | |
|-----|--------|---|-------|
| (1) | Udevu | - | Ndevu |
| (2) | Udago | - | Ndago |
| (3) | Udara | - | Ndara |
| (4) | Ubwana | - | Mbawa |

Katika ngeli hii kiambishi awali N cha wingi mara nyingine hujidhihirisha kwa alomofu M (mfano 4 hapo juu unahusika). Mabadiliko haya hutokana na sababu za kifonolojia ambazo hatuwezi kuzieleza katika makala haya.

6 Ngeli ya ya U - M

Mifano

- | | | | |
|-----|---------|---|----------|
| (1) | Ugonjwa | - | Magonjwa |
| (2) | Uasi | - | Maasi |

7. Ngeli ya nomino zilizo na Kiambishi Awali cha Umoja tu Pamoja na Mofu Kapa ya Wingi

Mifano

(1)	Upawa	-	ØPawa
(2)	Ukingo	-	ØKingo
(3)	Uchaga	-	ØChaga
(4)	Ukanda	-	ØKanda
(5)	Ufunguo	-	ØFunguo
(6)	Upande	-	ØPande
(7)	Ukucha	-	ØKucha
(8)	Ufuo	-	ØFuo
(9)	Ukuta	-	ØKuta
(10)	Upembe	-	ØPembe

8 Ngeli ya Nomino zilizo na Kiambishi awali cha wingi tu pamoja na Mofu kapa ya umoja

Mifano

(1)	Ødebe	-	Madebe
(2)	Økasha	-	Makasha
(3)	Øjembe	-	Majembe
(4)	Øbepari	-	Mabepari
(5)	Øbibi	-	Mabibi

9. Ngeli za Nomino zisizo na Kiambishi hata Kimoja

Nomino zilizo katika ngeli hii hazina kiambishi chochote. Maumbo ya nomino katika umoja na wingi yanafanana. Nomino hizi haziwekewi viambishi vyoyote vya idadi iwe ya umoja au ya wingi.

Mifano

(1)	Ndama	-	Ndama
(2)	Mbuzi	-	Mbuzi
(3)	Nguo	-	Nguo
(4)	Nyumba	-	Nyumba
(5)	Nyanya	-	Nyama

Tunakumbushwa hapa kuwa viambishi tulivyotumia katika uainishaji huu ni vile viambishi vya idadi ya umoja na idadi ya wingi. Tunasema, kwa mfano, kuwa nomino zilizo katika ngeli hii huwa haziwekewi viambishi vya idadi. Nomino hizi hazina

kiambishi cha umoja wala cha wingi. Lakini hatusemi kuwa nomino hizo haziwezi kuwekewa viambishi vilivyo na uamilifu tofauti na ule wa kuonyesha idadi. Nomino hizi, kwa mfano zinaweza kuwekewa viambishi vya kuzikuza au kuzifanya ndogo kwa mfano:

- | | | | |
|-----|--------|---|---|
| (1) | Ndama | - | jidama / jindama -kijiadama / kijindama |
| (2) | Mbuzi | - | jibuzi / jimбуzi, kijimбуzi / kijimбуzi |
| (3) | Nyumba | - | jumba / kijumba |
| (4) | Nyanya | - | jinyanya / kijinyanya |

Tanbihi: Katika kazi tulizozichambua hapo juu nomino hizi zimewekwa katika ngeli ya N - N. Mtazamo wetu haukubaliani na mgawanyo huo kwani hatuafiki kuwa N - N ni viambishi. Tunaamini ya kuwa nomino hizi hazina viambishi kwani maumbo ya umoja ni sawa na maumbo ya wingi yaani hayabadiliki. Sehemu isiyobadilika ni mzizi wa neno. Haiwezekani sehemu ya mzizi iwe kiambishi. Tunaamini ya kuwa mabadiliko mengine ambayo huiathiri Nomino ni mabadiliko ya kifonolojia tu na wala si ya kimofolojia.

Katika ngeli hii hii tunazo pia nomino ambazo zinalo umbo moja tu ama la umoja au la wingi - yaani hizi ni nomino zisizohesabika. Nomino hizi hufikiriwa ama katika umoja au katika wingi. Tunaamini nomino hizi nazo hazina kiambishi chochote.

Mifano

- | | | | |
|-----|--------|-----|--------|
| (1) | Hewa | (2) | maji |
| (3) | ukungu | (4) | mafuta |
| (5) | chai | (6) | maziwa |
| (7) | umande | (8) | mavi |
| (9) | kuimba | | |

Faida za Uainishaji wa Kimofolojia wa Ngeli

Aghalabu jukumu mojawapo la mwanaisimu yeyote huwa ni kufafanua lugha. Katika kutimiza lengo hilo mwanaisimu hulazimika kueleza ruwaza zozote zilizopo katika lugha anayoishughulikia. Kwa hiyo uainishaji huu unatusaidia katika:

- (1) Kutimiza lengo mojawapo la wanaisimu la kufafanua dhana ya ngeli za nomino kwa kutumia lugha ya Kiswahili.
- (2) Kuelewa ngeli za kimofolojia za nomino za Kiswahili. Hii ni finomena iliyopo na haiwezi kufumbiwa macho. Uainishaji huu unatusaidia sana kuelewa mofolojia ya nomino za Kiswahili.
- (3) Kuonyesha udhaifu uliojitokezea katika kazi za awali.

Hitimisho

Tumetumia kongoo la data kutokana na miainisho ya ngeli za nomino za Kiswahili kama iliyoainishwa na wanaisimu Krapf (1850), Madan (1884/1921), Ashton (1844), Brain (1969), Loogman (1867), Steere (1834), Polome (1967), na Myachina (1981). Tofauti, dosari, utenge, na makengenya mengi yamejitokeza katika miainisho hii. Baadhi ya dosari hizo (ingawa siyo zote) ni:-

1. Kwamba idadi ya ngeli za kimofolojia za nomino za Kiswahili inatofautiana sana miongoni mwa wanaisimu.
2. Kwamba, zipo tofauti kadhaa katika kuzipa majina ngeli za kimofolojia za nomino za Kiswahili.
3. Kwamba, zipo tofauti nyingi katika mfuatano wa ngeli za nomino za Kiswahili. Hatujui ipi ni ya kwanza, ya pili, ya tatu, n.k.
4. Kwamba, kuna tofauti kubwa ya nomino zinazowekwa katika ngeli fulani miongoni mwa wanaisimu.
5. Kwamba, upo uwezekano mkubwa wa kukosa mahali pa kuziweka nomino nyingi za kiswahili ambazo hazianzii na viambishi awali vilivyotumiwa kuainishia ngeli za kimofolojia za nomino za Kiswahili.

Mapendekezo yetu yameonyesha ya kuwa:

- (1) Zipo ngeli za: (i) M - WA (ii) JI - MA (iii) M - Mi (vi) KI - VI (v) U - N (vi) U - MA.
- (2) Ipo ngeli moja ya nomino zilizo na kiambishi awali cha umoja na kapa ya wingi. m. f. (1) Ukuta - Økuta. . . .
- (3) Ipo ngeli moja ya nomino zenye kiambishi awali cha wingi na kapa ya umoja. m.f. (1) Ødebe - madebe.
- (4) Ipo ngeli moja ya nomino zisizo na kiambishi awali chochote
m.f. samaki - samaki
kuku - kuku
- (5) Jumla tunazo ngeli za kimofolojia za nomino za Kiswahili zipatazo TISA.

MAKTABA
TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI

Marejeo

- Ashton, E.O. (1944). *Swahili Grammar Including Intonation*. London.
- Brain, B. (1969). *Basic structure of Swahili*, New York.
- Broomfield (1931) *Sarufi ya Kiswahili*, London
- Krapf (1850). *An Outline of the Elements of Kiswahili Language with special reference to the Kinika Dialect*, Tuebengnen.
- Loogman, A. (1865). *Swahili Grammar and Syntax*, Pittsburg.
- Madan, A.C. (1921). *Swahili (Zanzibar) Grammar* London.
- Meinhof, C. (1948). *Grundzuge Einer Vergleichenden Grammatik*.
- Mgullu, R.S. (1990). *The Structure of Kiswahili Sentences. A Transformational Approach*. (M.A: Dissertation), University of Nairobi.
- Myachina, *The Swahili Language A Descriptive Grammar*, London.
- Nida, E.A. (1949). Morphology. *The descriptive analysis of Words*, Michigan.
- Polome, E. (1967). *Swahili Language Handbook* Washington.
- Steere, E. (1834/1976). *Swahili Exercises*, OUP.
- TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*, Dar es Salaam.
- TUKI (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Dar es Salaam.